



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO**



**SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA
(COASCO)**

TANGAZO LA NAFASI ZA KUHAMIA KATIKA SHIRIKA LA COASCO

Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (**COASCO**) ni Shirika la Umma, lililoanzishwa kwa Sheria Na.15 ya mwaka 1982 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2005. Jukumu Kuu la Shirika ni kufanya ukaguzi wa nje (External Audit) kwa vyama vya ushirika nchini.

Shirika limepewa kibali na Serikali cha nafasi 12 za Watumishi wa Umma kutoka Taasisi zingine za Serikali kuhamia COASCO. Kibali hicho ni kwa watumishi wa umma wa Kada ya Ukaguzi (Audit Officer II) 10 na Kada ya Makatibu Mahsusi (Personal Secretary II) 2.

Hivyo Shirika linawatangazia Watumishi wa Umma ambao wanapenda kuhamia katika COASCO katika nafasi hizo, wenye sifa zifuatazo kwa kila Kada:

1. Afisa Mkaguzi Daraja la II (Nafasi 10)

a) Sifa za Mwombaji

Wenye shahada ya uhasibu na fedha katika masomo ya ukaguzi na uhasibu (Accounting and Finance) au kuwa na sifa sawa na hizo kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali.

b) Ngazi ya Mshahara: COASS 4

2. Katibu Mahsusi Daraja la II (Nafasi 2)

a) Sifa za Mwombaji

Wenye cheti cha elimu ya Sekondari (CSEE) na kufaulu katika masomo ya Kiingereza na Kiswahili pamoja na kuwa na cheti cha Diploma ya Katibu Mahsusi (Diploma in Secretarial Course) na kufaulu Hati Mkato (Kiingereza) na Hati Mkato (Kiswahili) kwa kasi ya maneno 80 kwa dakika na kuwa na cheti cha weledi wa kompyuta katika (MS-Word, MS-Excel, Internet, Email, MS-Publisher) kutoka katika chuo kinachotambulika na Serikali.

b) Ngazi ya Mshahara: COASS 2

JINSI YA KUOMBA

Watumishi wa Umma wenye nia ya kuomba hawana budi kuwasilisha barua za maombi zikiambatana na:

- i) Taarifa binafsi (CV) zikiwa na majina na anwani pamoja na namba za simu.
- ii) Nakala za vyeti vya masomo vilivyothibitishwa (Certified).

ANGALIZO:

- i) Waombaji lazima wapitishie barua za maombi kwa waajiri wao wa sasa kwani kutofanya hivyo, maombi yao hayatafikiriwa.
- ii) Waombaji wote waoneshe nafasi ya kazi wanayoomba juu ya bahasha.
- iii) Waombaji watakaokidhi vigezo na kufaulu usaili ndiyo watakaojulishwa kwa hatua zinazofuata.
- iv) Waombaji wathibitishie utayari wa kujigharamia uhamisho huo.

Maombi yawasilishwe ndani ya siku kumi na nne (14) tokea tarehe ya tangazo hili kupitia anwani ifuatayo:

Mkurugenzi Mkuu,
Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO),
S. L. P. 761,
DODOMA.

Au

Kwa barua pepe: info@coasco.go.tz

**Limetolewa leo tarehe
27 Juni, 2022**